

Haki zako kama Mteja wa Idara ya Ulemavu wa Makuzi

Your rights as a client of the Developmental Disabilities Administration

Haki zilizoainishwa hapo chini ni haki za kiwango cha chini kabisa zinazohakikishwa kwa wateja wa idara, na hazilengi kuhafifisha haki zilizoainishwa katika majimbo mengine au sheria za serikali kuu ambazo zinaweza kuwa na haki nyingine.

(1) Idara inapaswa kumtaarifu mhusika na mwakilishi halali wa mhusika au mwakilishi wa makazi muhimu ya ziada kuhusu haki zilizoainishwa katika sura 71A. RCW, sheria ya mwaka 2020 baada ya kubaini mhusika ni mtu mwenye ustahili. Taarifa zinazotolewa na idara zinapaswa kuwa za kimaandishi. Idara inapaswa kuandika kumbukumbu ya tarehe ambayo taarifa inayohitajika katika kifungu hiki kidogo ilitolewa.

(2) Idara inapaswa kumtaarifu mhusika na mwakilishi halali wa mhusika au mwakilishi wa makazi muhimu ya ziada kuhusu haki zilizoainishwa katika sura 71A. RCW, sheria ya mwaka 2020 baada ya kubaini mhusika ni mtu mwenye ustahili. Taarifa zinazotolewa na idara zinapaswa kuwa za kimaandishi. Idara inapaswa kuandika kumbukumbu ya tarehe ambayo taarifa inayohitajika katika kifungu hiki kidogo ilitolewa.

(3) Mteja ana haki ya kujitegemea na kuchagua kuwa huru kutoingiliwa na mtoa huduma. Hii inajumuisha haki ya mteja ya:

- (a) Kuwa huru dhidi ya unyanyasaji wa kingono, kimwili, na kiakili, adhabu za viboko, na kutengwa bila hiari;
- (b) Kuwa huru dhidi ya ubaguzi kwa minajili ya mbari, rangi, imani, utaifa, dini, jinsia, umri, ulemavu, hali ya ndoa na familia, utambulisho wa kijinsia, au mwelekeo wa kingono;
- (c) Kufanya chaguzi kuhusiana na aina ya chakula kilichopo katika rasilimali za mteja na mpango wa huduma;
- (d) Kuwa na wageni nyumbani kwa mteja na kuhusiana na watu anaowachagua mteja mwenyewe na kuwa na mipaka kama yalivyo mapatano na wakazi wenza wa mteja;
- (e) Kudhibiti ratiba ya mteja na kuchagua shughuli, ratiba, na huduma ya afya inayokidhi mahitaji ya mteja;
- (f) Taarifa kuhusu matibabu yaliyooombwa na mtoa huduma ya afya wa mteja na mpango wa usaidizi jinsi matibabu yatakavyofanywa.
- (g) Kuwa huru dhidi ya dawa zisizo muhimu, vizuizi na makatazo;
- (h) Kupiga kura, kushiriki katika mchakato wa kidemokrasia, na kuwasaidia watu kuchaguliwa kushika madaraka;
- (i) Kusimamia fedha za mteja au kuchagua mtu wa kusaidia hilo;
- (j) Kuwa sehemu ya jumuiya;
- (k) Kufanya maamuzi kuhusu maisha ya mteja;
- (l) Kuchagua nguo na mtindo wa nywele anaoutumia mteja;
- (m) Kuweka samani na kupamba chumba cha kulala cha mteja kulingana na mapendeleo ya mteja au kuweka samani na kupamba nyumba ya mteja kulingana na mapendeleo ya mteja kulingana na makubaliano na wakazi wenza wa mteja;
- (n) Kutafuta ajira yenye malipo;
- (o) Kupokea huduma ambazo mteja anakubali kuzipokea;
- (p) Kuamua kushiriki au kutoshiriki katika utafiti baada ya utafiti kutolewa maelezo kwa mteja, na baada ya mteja au mwakilishi halali wa mteja kutoa ridhaa ya kimaandishi ya mteja huyo kushiriki kwenye utafiti; na
- (q) Kuwa huru dhidi ya unyonyaji wa kifedha.

(4) Mteja ana haki ya kushiriki katika uwekaji mipango ya huduma za idara. Hii inajumuisha haki ya mteja ya:

- (a) Kushiriki na kutoa maoni kuhusu mipango ya huduma za mteja iliyoandikwa na idara na watoa huduma;
- (b) Kuwa na fursa zenye tija za kuongoza michakato ya uwekaji mipango;
- (c) Kuhakikisha maoni ya mteja ya maisha yenye tija na malengo ya mteja ya elimu, ajira, nyumba, mahusiano, na burudani yajumuishwa kwenye mchakato wa uwekaji mipango;
- (d) Kuchagua wakili wa kuhudhuria michakato ya uwekaji mipango pamoja na mteja; na
- (e) Kufikia taarifa za sasa na zilizo sahihi kuhusu fursa za burudani, elimu, na ajira zilizopo kwenye jumuiya ya mteja.

- (5) Mteja ana haki ya kufikia taarifa zinazohusu huduma na matibabu. Hii inajumuisha haki ya mteja ya:
- (a) Kutazama nakala ya mipango yote ya sasa ya huduma;
 - (b) Kumiliki nakala kamili za mipango ya sasa ya mteja;
 - (c) Kufanya mapitio ya sera na taratibu za huduma yoyote anayopokea mteja, wakati wowote. Hii inajumuisha sera na taratibu kuhusu jinsi mteja anavyoweza kufungua malalamiko kwa watoa huduma na idara;
 - (d) Kuchunguza matokeo ya utafiti wa hivi karibuni wa idara au ukaguzi uliofanywa na watafiti au wakaguzi wa serikali, matamko ya upungufu, na mipango ya masahihisho yaliyofanywa kuhusiana na mtoa huduma wa mteja na makazi ya mteja. Mtoa huduma wa mteja anapaswa kumsaidia mteja kutafuta na kufikia taarifa kama mteja akiomba hivyo, na
 - (e) Kupokea taarifa za kimaandishi za hatua za kisheria zilizochukuliwa na idara dhidi ya mtoa huduma wa mteja. Meneja wa kesi wa idara au mteule wake anapaswa kutoa taarifa kwa mteja na mwakilishi halali wa mteja au mwakilishi wa makazi muhimu ya ziada ndani ya siku ishirini na moja, bila kuhesabu siku za mwisho wa wiki na sikukuu, za taraha ya uchukuaji hatua za kisheria. Kwa dhumuni la kifungu hiki kidogo, "mtoa huduma" anamaanisha mhusika anayetoa huduma za makazi zinazopokelewa na mteja ambazo zinaendeshwa au kupatikana kupitia idara. Hatua za kisheria zinazohitaji taarifa hii zinajumuisha:
 - (i) Masharti yaliyowekwa kwenye cheti au leseni ya mtoa huduma;
 - (ii) Kusimamishwa au kusimamishwa kiasi kwa rufani au mapokezi;
 - (iii) Kupewa cheti au kufutiwa cheti cha utoaji wa huduma; au
 - (iv) Kukataliwa, kusimamishwa, au kubatilishwa kwa leseni au cheti.
- (6) Mteja ana haki ya kufungua malalamiko na lawama, na kukata rufaa. Hii inajumuisha haki ya mteja ya:
- (a) Kukata rufaa ya uamuzi wowote wa idara ambao unakataa, unapunguza, au kusitisha ustahili wa mteja, huduma, au chaguo la mtoa huduma kama ilivyofasihiwa kwenye sheria ya serikali kuu ya Medicaid na sheria za nchi za usaidizi wa umma;
 - (b) Kutoa lawama kwa mtoa huduma wa mteja kuhusu huduma za mteja au wasiwasi mwingine. Hii inajumuisha, lakini haikomei kwa, wasiwasi kuhusu tabia ya watu wengine mahali ambapo mteja anaishi. Mtoa huduma anapaswa kudumisha sera ya kimaandishi kuhusu mchakato wa lawama unaojumuisha ratiba ya muda na malipo yanayoweza kupatikana. Kama lawama haitatatuwa, mtoa huduma anapaswa kumpa mteja taarifa kuhusu jinsi ya kuwasilisha lawama kwa idara;
 - (c) Kufungua malalamiko na lawama, na kukata rufaa bila ya kuadhibiwa au kufanyiwa malipizi kutoka kwa idara au watoa huduma; na
 - (d) Kupokea taarifa kuhusu jinsi ya kupata makazi kwa ajili ya walemavu katika mchakato wa rufaa.
- (7) Mteja ana haki ya ufaragha na usiri. Hii inajumuisha haki ya mteja ya:
- (a) Ufaragha na usiri wa rekodi binafsi za mteja;
 - (b) Kuwasiliana kwa ufaragha, ikiwemo haki ya kutuma na kupokea barua na barua pepe, na haki ya kutumia simu kwenye eneo ambalo simu inaweza kutumika bila kusikiwa na wengine; na
 - (c) Kukutana na kuongea kwa ufaragha na rafiki na wanafamilia wa mteja.
- (8) Mteja ana haki wakati wa kuruhusiwa, kuhamishwa, na kusitishwa kwa huduma kama zilivyoainishwa kwenye kifungu hiki kidogo.
- (a) Wateja ambao ni wakazi wa kituo cha malezi ya muda mrefu ambacho kina leseni kwa mujibu wa sura [18.20](#), [72.36](#), au [70.128](#) RCW wana haki zilizoainishwa katika [RCW 70.129.110](#).
 - (b) Wateja ambao wanapokea huduma za makazi ya jumiya ambazo zimethibitishwa kisheria wana haki ya:
 - (i) Kubaki na mtoa huduma wa mteja. Huduma hazipaswi kusitishwa isipokuwa mtoa huduma anabaini na anasema kwamba:
 - (A) Mtoa huduma hawezi kukidhi mahitaji ya mteja;
 - (B) Usalama wa mteja au usalama wa watu wengine kwenye kituo au makazi upo hatarini;
 - (C) Afya ya mteja au afya ya watu wengine kwenye kituo au makazi inaweza kuwa hatarini; au
 - (D) Mtoa huduma anaacha kuendesha shughuli husika.

(ii) Anapokea notisi ya kimaandishi kutoka kwa mtoa huduma ya uwezekano wowote wa kusitishwa kwa huduma angalau siku thelathini kabla ya usitishaji huo, isipokuwa kama kuna dharura ya kiafya au ya kiusalama ambayo inahitaji kusitishwa kwa huduma, ambapo notisi itatolewa angalau saa sabini na mbili kabla ya tarehe ya usitishaji. Notisi hiyo inapaswa kutolewa kwa mteja na mwakilishi halali wa mteja au mwakilishi wa makazi muhimu ya ziada. Notisi hiyo inapaswa kujumuisha:

- (A) Sababu ya kusitishwa kwa huduma; na
- (B) Tarehe rasmi ya kusitishwa kwa huduma.

(iii) Kupokea mpango wa mpito angalau siku mbili kabla ya tarehe rasmi ya kusitishwa kwa huduma, au kama usitishaji huo ulitokana na dharura ya kiafya au ya kiusalama kupokea mpango wa mpito ndani ya siku mbili baada ya idara kupokea notisi ya usitishaji kutokana na dharura. Idara inapaswa kumpatia mteja na mwakilishi halali wa mteja au mwakilishi wa makazi muhimu ya ziada mpango husika. Mpango huo unapaswa kujumuisha:

- (A) Eneo ambalo mteja atahamishwa;
- (B) Njia ya usafiri kwenda eneo jipya; na
- (C) Jina, anwani, na nambari ya simu ya mtetezi wa ulemavu wa makuzi.

(c) Mtoa huduma anayetoa huduma kwa wateja kwenye makazi yanayomilikiwa na mtoa huduma anapaswa kutoa taarifa za kutosha kuhusu taratibu za kusitishwa kwa huduma kabla ya kuanza kwa hatua yoyote ya kuweka kizuizini kinyume na sheria kwa mujibu wa [RCW 59.12.030](#).

(9) Mteja ana haki ya kuwa na mawakili. Mteja ana haki ya kupokea taarifa kutoka kwa mashirika yanayotenda kama mawakili wa mteja, na kupewa fursa ya kuwasiliana na mashirika haya. Mtoa huduma hapaswi kuingilia ufikio wa mteja wa yoyote ya mambo yafuatayo:

- (a) Mwakilishi yoyote wa serikali;
- (b) Daktari binafsi wa mkazi husika;
- (c) Mtetezi wa masuala ya ulemavu wa makuzi; au
- (d) Mwakilishi yoyote wa shirika lililochaguliwa kutekeleza programu ya ulinzi na utetezi kwa mujibu wa [RCW 71A.10.080](#).

(10) Kama mteja yuko chini ya amri ya ulezi kwa mujibu wa sura [11.88 RCW](#), haki za mteja chini ya sura 71A. RCW, sheria ya mwaka 2020 zinatekelezwa na mlezi wa mteja kama suala husika lipo ndani ya wigo wa amri ya ulezi.